JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Mkuu wa Shule 0692475406**
**Makamu Mkuu wa Shule 0713007642**
**Patron: 0684752221**
**Shule ya Sekondari Kongwa**
**S.L.P 16**
**Kongwa**

**12 June, 2023.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .............**
**.....................................................**
**S.L.P ..........................................**
**....................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KONGWA HALMASHAURI YA KONGWA MKOA WA DODOMA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ......................

Shule ya Sekondari Kongwa ipo umbali wa Kilometa 86 Mashariki mwa Jiji la Dodoma. Usafiri wa basi kutoka Jiji la Dodoma unapatikana katika kituo cha mabasi Job Ndugai Jijini Dodoma. Nauli ni Shilingi 5,000/= kwa basi kutoka Jijini Dodoma hadi kituo cha mabasi cha Kongwa.Kutoka kituo cha mabasi cha Kongwa mpaka shuleni nauli ni shilingi 1,000/= kwa pikipiki

Kwa wanaotoka Mkoa wa Dar es salaam kituo cha kushukia ni Mbande na atapanda daladala ya kutoka Mbande kuja Kituo cha Kongwa kwa nauli TSh 2,000/= tu.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/8/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/8/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/8/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

(a) Mashati mawili (02) au zaidi meupe ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja.Inashauriwa mashati aina ya tomato ndiyo yanafaa zaidi.Shati lazima lioneshe namba tano ya Kirumi "V" kwenye mabega yote mawili (kwa kutumia kitambaa cha suruali) itakayosomeka kwa mabele.

(b) Suruali mbili (02) au zaidi za rangi dark bluu zilizoshonwa vizuri zenye marinda mawili kwa mbele na mfuko mmoja wa nyuma usio na zipu na pindo la chini (turnup) lenye upana wa inchi 15 (suruali za kubana yaani modo haziruhusiwi) na mkanda mweusi. Upana wa chini wa suruali utapimwa wakati wa kuripoti

(c) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali..

(d) Viatu vya shule ni nyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

(e) Sweta rangi ya dark bluu.

(f) Soksi nyeupe jozi mbili (02) au zaidi.

(g) Sare za michezo ni tracksuit za bluu zenye mistari myeupe mikononi na zisizo na maandishi,T-shirt ya bluu ya timu ya taifa ya Tanzania na bukta yake.

(h) Viatu vya michezo (raba na viatu vya mpira wa miguu)

(i) Nguo za kushindia (shamba dress) suruali nyeusi mbili na fulana (Tshirt) moja au zaidi,zinapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 15,000/= kwa kila moja na suruali nyeusi.

(j) Viatu vya wazi (sandals) kwa ajili ya kushindia na kandambili kwa ajili ya kuogea.

(k) Mzazi unashauriwa kumapatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

**ZINGATIA:** Nguo ambazo sio zare ya shule yaani ambazo hazijaandikwa kwenye fomu hii haziruhusiwi shuleni.
Ukaguzi wa vifaa/vitu vyote utafanyika siku ya kuripoti.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12 counter book quire 4.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma PCB na HGL waje na Advanced learners' Dictionary iwe imeandikwa Oxford, kwa ajili ya matumizi yake.
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma PCB Na HGL
vi. Godoro liwe na ukubwa kipimo cha 6 X 2½
vii. Mashuka Jozi 2 ya rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 ya bluu;
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Jembe lenye mpini moja na soft bloom moja kwa wanafunzi wote.
xii. Panga 1 na squizer 1 kwa wanafunzi wa PCB
xiii. Fagio 1 la chelewa lenye mpini na kwanja 1 au reki 1 kwa wanafunzi wa HGL
xiv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa na hati ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
xv. Sanduku la bati imara (Tranker) lenye makufuli mawili.

**ANGALIZO:**

**(a)** Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni.Aje na tranka moja tu.

(b) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote atakapokuwepo shuleni isipokuwa kwa wito kama italazimika.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

**5.**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KONGWA**

Headmaster
Kongwa Secondary School
P.O.Box 16 Kongwa

...................................

**ALEX A. SALUM**
**MKUU WA SHULE**

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ANDIKA KWA HERUFI KUBWA)**

JINA KAMILI ......................................................................................... (MAJINA MATATU)

SHULE YA SEKONDARI ULIYOTOKA...........................................................................

WILAYA ...........................................................
MKOA...........................................................

ANWANI YA ULIKOTOKA.....................................................................................
............

TAREHE YAKUZALIWA.......................................................................................
..................

JINA KAMILI LA BABA ....................................NAMBA YA SIMU................

JINA KAMILI LA MAMA ....................................NAMBA YA SIMU................

UHUSIANO WAKO NA MLEZI.......................................

TAJA NDUGU WATATU WA KARIBU WATAKAOFIKA SHULENI PINDI JAMBO LOLOTE LIKITOKEA LINALOMHITAJI MZAZI AU MLEZI IKIWA HAWAPO

1. ..................................................................
   S.L.P...........................................................
   NAMBA YA SIMU ....................................
   UHUSIANO ..............................................

2. ..................................................................
   S.L.P...........................................................
   NAMBA YA SIMU ....................................
   UHUSIANO ..............................................

3. ..................................................................
   S.L.P...........................................................
   NAMBA YA SIMU ....................................
   UHUSIANO ..............................................

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KONGWA**

A: Mimi ................................................................................ ( majina matatu kwa herufi

kubwa) wa S.L.P. .................................. nimeyaona na

kuyasoma maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari Kongwa,

nimeelewa vema , nami naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati

wote kujifunza kwa bidii ili nipate elimu bora ambayo itakuwa ni

kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Saini...........................................

Tarehe........................................

B: Mimi ...................................................................(majina matatu kwa herufi kubwa)

mzazi/mlezi wa

...........................................................................nimeyaona na

kuyasoma maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Kongwa ,

naahidi kumsaidia kwa hali na mali ili niweze kukamilisha elimu ya

sekondari . Nitashirkiana na uongozi ili kutimiza azma hii.

Saini ...................................

Tarehe .................................

MEDICAL EXAMINATION FORM (FOMU YADAKTARI)
FROM THE HEAD MASTER , KONGWA SECONDARYSCHOOL

TO THE MEDICAL OFFICER,
.....................................................
NAME OF STUDENT : ............................................
AGE: ............................................................................

| MEDICALHISTORY | YES | NO |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Pepticulcers | | |
| Epilepsies | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidneyproblem | | |
| Anemia | | |
| Neurosis | | |

PhysicalExamination

1. Respiratorysystem
2. Cardio vascularsystem
3. Urinarysystem
4. Reproductivesystem
5. Eye
6. E.N.

Investigate

1. Blood-HB................................................
   WBC............................................
   ERS..............................................
   VDRL Test ............................
2. Urine - Sed...................................
   Stool...................................

I have examined and consider that he is physical and mental fit/unfit for

further education Signature

......................................................... Date ...........................